**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**
**CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION**

**015/1** **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 1**
(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

**Muda: Saa 2** **Jumatatu, 10 Novemba 2014 mchana**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **yote.**
3. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
4. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.





Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

## SEHEMU A (Alama 10)
## SUNNAH NA HADITH

1. Chagua jibu sahihi katika kipengele (i) – (x) kisha andika herufi yake katika kijitabu chako cha kujibia.

(i) Maelezo yapi yanatoa maana ya Hadith za Mtume (s.a.w)?
- A Simulizi (mapokeo) au taarifa juu ya Mtume (s.a.w)
- B Taarifa juu ya mwenendo wa Mtume (s.a.w)
- C Simulizi juu ya yale aliyoagiza Mtume (s.a.w) yafanywe na aliyoyakataza
- D Habari za Mtume (s.a.w) zilizosimuliwa na masahaba wake
- E Taarifa na simulizi za masahaba ambazo Mtume (s.a.w) aliziusia.

(ii) Kauli inayoonesha matumizi mabaya ya neno "Sunnah" ni
- A Dawa za Sunnah
- B Swala za Sunnah
- C Funga za Sunnah
- D Sunnah za kuoa
- E Sunnah za udhu.

(iii) Njia kuu zilizotumika kuhifadhi Sunnah wakati wa Mtume ni
- A kuigiza na kukaa pamoja na Mtume
- B kuhifadhi vifuani na katika matendo
- C kwa maandishi na kuhifadhi vifuani
- D kuzifundisha na kuzisoma mara kwa mara
- E kusimulia na kufanya majadiliano.

(iv) Maelezo yanayoonesha tofauti kati ya hadithi Qudussiyyi na hadithi Nabawiyyi ni
- A Qudussiyyi zimo katika vitabu wakati Nabawiyyi zimo vifuani
- B Qudussiyyi zipo nyingi zaidi katika vitabu vya hadithi kuliko Nabawiyyi
- C Nabawiyyi ni kauli ya Allah wakati Qudussiyyi ni mawazo ya Mtume
- D Qudussiyyi ina Matin ya Qur'an wakati Nabawiyyi ina Matin ya Mtume
- E Nabawiyyi ni mashuhuri zaidi kuliko Qudussiyyi.

(v) Hadithi sahihi zaidi ni ile iliyonukuliwa kutoka kitabu cha
- A Sahih Bukhar na at-Tirmidh
- B Sahih Bukhar na Sahih Muslim
- C Sahih Muslim na Sunan Abu Daud
- D Sunan Abuu Daud na Musnad ya Ibn Hambal
- E At-Tirmidh na Sunnah ya Ibn Majah.

(vi) Kufuata Sunnah ni wajibu kwa kila Muislamu kwa sababu
- A ya kusimamisha Uislamu katika jamii
- B ni msingi wa kwanza wa sheria ya Kiislamu
- C ni sheria ya Allah (s.w) yenye kugusa nyanja zote za maisha
- D ni kioo cha Uislamu wa watu
- E kunamfanya mtu kuwa mcha Mungu.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

**SEHEMU E (Alama 30)**
**TAREKH**

5. Chagua **neno** au **kifungu cha maneno** (i) – (xxx) ili ukamilishe kauli (a) – (o) kwa usahihi. Maneno au vifungu vya maneno vinaweza kutumika zaidi ya mara moja.

(i) Umayyah
(ii) Bibi Sauda (r.a)
(iii) Abu Bakar (r.a)
(iv) Ali (r.a)
(v) Ikhwaanul-Muslimiin
(vi) Shuayb (a.s)
(vii) Sayyid Abul-Ala Maudud
(viii) Hajrah
(ix) Jibril na Mikail
(x) Ummar (r.a)
(xi) Abdallah bin Sabaa
(xii) Fat-h-Makka
(xiii) Adam (a.s) na Hawa
(xiv) Zayyid
(xv) Is-haqa
(xvi) Nuhu (as)
(xvii) Madina
(xviii) Ibrahim (a.s)
(xix) Uthman (r.a)
(xx) Abu Ayyub (r.a)
(xxi) Al-muwatta
(xxii) Shahiid Hassan Al-Bannah
(xxiii) Miraj
(xxiv) Sarah
(xxv) Jamiatil-Islamy
(xxvi) Namrudh
(xxvii) Ibilisi
(xxviii) Harith
(xxix) Bibi Aysha (r.a)
(xxx) Iman Malik bin Anas

**Maswali**

(a) Mnafiki ajulikanaye kwa jina la _________ alieneza fitna kubwa katika Uislamu wakati wa Ukhalifa wa __________.
(b) Mama yake Is-haqa (a.s) alijulikana kwa jina la __________ wakati mama wa Ismail (a.s) aliitwa __________.
(c) Katika ukumbi wa Thaqifah Bani Saidah, ___________ na Saad bin Ubaidah walimpendekeza __________ ili ashike ukhalifa wa dola ya kiislamu.
(d) Tunatakiwa kujihadhari na ____________ kwani hadaa zake ziliwafanya ___________ wakavunja amri ya Allah (s.w).
(e) Israa na __________ ni safari ya Mtume (s.a.w) iliyofanyika mwaka wa 12 H chini ya uongozi wa __________.
(f) Nabii __________ alitumwa kwa watu wa __________ waliokithiri katika kupunja mizani.
(g) Nabii__________ alikabiliana na mfalme __________ kwa hoja katika kuonesha upweke wa Allah (s. w).
(h) Kukataa __________ na kumuua ngamia wa __________ kwa jeuri kulisababisha kuangamizwa kwa watu wa Thamud.
(i) __________ ni mtoto wa __________ aliyezaliwa wakati wazazi wake wote wawili wakiwa wazee sana.
(j) Kuuwawa kwa__________ ilikuwa ni matokeo ya fitina iliyoanzishwa na __________ ambaye alikuwa Myahudi aliyesilimu uongo.
(k) Mtume (s.a.w) alikaa katika nyumba ya __________ pamoja na mkewe ___________ mjini Yathrib.
(l) Vita vya ngamia ilikuwa ni mapambano kati ya jeshi lililoongozwa na ___________ dhidi ya jeshi lililoongozwa na __________.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

(m) __________ ni mmoja wa wasomi mashuhuri aliyeandaa kitabu cha hadith kilichoitwa __________.

(n) __________ ni kundi la harakati lililoasisiwa na mwanaharakati __________ kwa lengo la kuhuisha Uislamu nchini Misri.

(o) __________ ni kikundi cha kuhuisha Uislamu kilichoanzishwa na kuendesha harakati za Kiislamu chini ya __________ nchini Pakistani.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner